

CoFUTURES

CoFUTURES ni kikundi cha utafiti cha kimataifa kinachojishughulisha na mustakabali wa ulimwengu miaka ijayo, sayansi ya kubuniwa (science fiction), na fikra za mambo ya baadae. Tunatumia sayansi ya kubuniwa, mawazo yatokanayo na dhana, na elimu ya miaka ya baadae ili kutatua changamoto mbalimbali duniani hivi sasa: mabadiliko ya hali ya hewa, mabadiliko ya teknolojia, na mabadiliko ya idadi ya watu.

CoFUTURES inaamini ya kwamba ili kuweza kuelewa vyema mambo ya mbeleni, aidha yawe ya kibinadamu, ya kuhusu spishi zingine, teknolojia au ya ulimwengu, ni lazima tujihusishe kutazama namna watu wanavyofikiria juu ya wakati ujao maeneo yote duniani. Lengo letu ni kuboresha uhusiano kati ya mawazo ya ndani na mawazo ya duniani katika kusaidia kutatua changamoto za ulimwenguni. Tunatazama suala la uendeleu kwa jicho tofauti na la kipekee. Tunachunguza maono ya uvumbuzi, na maono yasiyo ya kiasili ya mambo yajayo, pamoja na maswali ya haki za mazingira haswa kutoka katika mtazamo wa jamii zilizokataliwa na zilizotengwa.

CoFUTURES ipo mjini Oslo huku shughuli zake nyingi zikiwa zimetawanyika katika jamii mbalimbali, makundi ya tafiti na mitandao duniani kote. Inajihusisha katika utafiti ndani ya sekta mbalimbali ikiwemo tafiti za kinadharia, tafiti za kiteknolojia, tafiti za kisera, na tafiti za kisanaa. Lakini pia inatengeneza na kusimamia kazi za kisanaa za vyombo vya habari ikiwemo za kubuniwa, filamu na michezo ya video.

Miradi mikuu ya CoFUTURES ni:

1. *CoFUTURES: Njia kuelekea Nyakati Zinazowezekana*. Mradi huu umepokea ufadhili kutoka Baraza la Utafiti Ulaya (European Research Council) chini ya programu ya mpango wa ruzuku kwa ajili ya utafiti na uvumbuzi ya Umoja wa Ulaya iitwayo 'Horizon 2020'.
2. *Ubuniwaji wa Sayansi*: Mradi huu umepokea ufadhili kutoka Baraza la Utafiti la Kinorwei (Norwegian Research Council) chini ya FRIPRO-YRT.

Mradi huu unaendeshwa na Idara ya Mafunzo ya Utamaduni na Lugha za Mashariki (Department of Culture Studies and Oriental Languages), Chuo Kikuu cha Oslo.

Bodhisattva Chattopadhyay ni mchunguzi mkuu wa CoFUTURES. Anafanya kazi kama mtafiti wa sayansi ya kubuniwa, mkalimani, na mhariri. Ni mwandishi au mkalimani wa vitabu sita, vingi zaidi vinavyohusu sayansi ya kubuniwa, na pia ni moja wa waanzilishi na mhariri mwenza wa mfululizo wa kitabu cha *Studies in Global Genre Fiction* (Routledge). Yeye pia ni Profesa Msaidizi katika Mafunzo ya Utamaduni ya Ulimwenguni katika Chuo Kikuu cha Oslo.

Mawasiliano:



Bodhisattva Chattopadhyay



Department of Culture Studies, University of Oslo, Postboks 1010 Blindern, 0315 Oslo, Norway



bodhi@bodhisattvac.com



<http://cofutures.org>

